


A F R I

TWENDE

Kulitia moyo kanisa la Afrika katika kazi ya umisheni ulimwenguni



Jarida la 2, Toleo la 1

WWW.AFRIGO.ORG/AFRITWENDE

TUMIA UJUZI NA STADI KATIKA UMISHENI
WAOMBEE WATOPOSA WA SUDANI YA KUSINI

VIPAJI, STADI, KAZI
ZANA MIKONONI MWA MUNGU

YALIYOMO



04



06



08

03 MAONI YA MHARIRI (TAHARIRI)

04 KUTUMIA STADI NA UJUZI KATIKA UMISHENI

Watu wengi hutumia vipawa au kazi zao kwa ajili ya injili. Soma kuhusu mwalimu wa mpira wa pete, daktari wa mifugo, mfanyakishara na msanifu wa majengo ambaye hutumia ujuzi wake kwa ajili ya umisheni.

06 MTAZAMO: ITAKUWAJE WEWE KAMA MUNGU AKIKUITA UWE MSANIFU WA MAJENGO?

Ukinzani wa uongo unaonesha kwamba wale wenye taaluma za maarifa ya duniani hawana wito na hawawezi kujihusisha na huduma za kikristo.


07 NENDAI HABARI YA KANISA LA AFRIKA LINALOHAMASISHA UMISHENI

08 MAKUNDI YA WATU: WATOPOSA

Ni kundi la watu wanapatikana Sudanii ya Kusini na Ethiopia. Watu hawa wanaweza kufikiwa na injili kama watumishi watatumia taaluma zao za utabibu, udaktari wa mifugo, maendeleo ya kilimo na maji.

MAONI YA MHARIRI

UJUZI NA STADI KWA AJILI YA IBADA



Bwana akanena na Musa, na kumwambia, Angalia, nimemwiita kwa jina lake Bezaleli mwana wa Uri, mwana wa Huri, wa kabilia ya Yuda; tena, tazama, nimemchagua, awe pamoja naye, huyo Ohaliabu, mwana wa Ahisamaki, wa kabilia ya Dani; nami nimetima hekima katika miyo yo wote wenye moyo wa hekima, ili wapate kufanya vyote nilivyoquagiza; yaani, hema ya kukutania na sanduku la ushuhuda, na kiti cha rehemaa kilicho juu yake, na vyombo vyote vya Hema, (Kutoka 31:1-2,6-7).

Watu wengi huona vipawa vyao na ujuzi wao kama tu njia ya maisha ya kawaida ya kujipatia mkate wa kila siku. Kutumia ujuzi wetu kujipatia maisha mazuri, kwa ajili ya familia zetu na kuishi maisha bora ni lengo la kawaida. Hakuna kitu kibaya na kusudi hili. Swali ni kama tumetengenezwa tu kwa ajili ya kufurahia maisha yetu au kwa ajili ya kusudi kubwa zaidi. Je, maarifa na ujuzi wetu ni kwa ajili ya kujipatia kipato au ni kwa ajili ya ibada?

Katika kitabu cha Kutoka, Mungu anamwelekeza Musa kujenga hema mahali ambapo uwepo wake ungekaa na katika eneo ambalo watu wake wangeweza kumwabudu. Kazi hiyo ingehtaji vifaa muhimu vya ujenzi, lakini pia ufundi stadi wa hali ya juu kabisa. Musa angewezaje kupata ufundi stadi hu? Vema, Mungu alikuwa na jibu.

Kujenga Hema la Kibinadamu
Kuna masomo kadhaa kutoka katika kifungu hiki cha maandiko yanaendana

na kazi za umisheni wa leo. Kwanza, Mungu ndiye Mwanzilishi wa kazi yote ndani yetu na huifanya kupitia sisi na ndiye mtoaji wa stadi na vipawa – hata vile ambavyo tungeweza kufikiri tumevipata kwa nguvu zetu wenye. Kusema kweli Bezaleli na Ohaliabu walifanya kazi kwa bidi ili kuwa mafundi stadi. Hata hivyo, Mungu aliwaambia hakuwaita wao na kuwateua katika kazi hiyo tu, bali pia amewapa uwezo wa kupata stadi hizo: ‘nami nimemjaza roho ya Mungu, katika hekima, na maarifa, katika ujuzi, na mambo ya kazi ya kila aina, (Kutoka 31:3).

Kisha Mungu aliwapa wengine stadi ili wajijunge na kazi hii. Na mwisho, watu wa Mungu walikuwa na moyo wa kutoa vifaa vya ujenzi vilivyohitajika. Bezaleli na Ohaliabu, pamoja na wana wa Israeli walitambua kuwa vipawa vya Mungu na maarifa havikutolewa kwa ajili manufaa yao tu. Vilitolewa kwa ajili ya ibada na kwa kujenga hema la Mungu.

Bwana angali akiwaita watu wenye maarifa na stadi tofauti tofauti ili kutumika katika kazi yake ya mahema ya kibinadamu, yaani makazi ya Roho Mtakatifu. Anawazawadia watu na vipawa mbalimbali vya kiroho na aina zote za maarifa kwa ajili ya kazi hii. Anawatumia wale wenye uwezo katika udaktari wa binadamu, uhandisi, uhasibu, theolojia, elimu, sheria, ujenzi, kilimo, ufundi bomba, uuguzi, kompyuta na nyinginezo! Stadi hizi zimetoka kwa Bwana ili kila mmoja wetu aweze kuzitumia kumfanya Mungu ajulikane. Stadi hizi zinaweza

kugeuzwa kwa ajili ya Mwokozi kwa ajili ya wale ambao isingekuwa hivyo wasingeweza kuishi na kufa bila kusikia habari njema za Bwana Yesu.

Mungu anatumia wanataaluma

Miaka 21 iliyopita, mimi na mke wangu, Joanna tuliamua kutumia ujuzi na stadi zetu katika udaktari wa binadamu kwa ajili ya kazi ya Mungu ya umisheni ulimwenguni. Tumekuwa tukibarikiwa kumwona Mungu anavyotumia hiyo sadaka ndogo katika maisha ya wagonjwa na familia zao katika umisheni wa kutoa huduma hospitalini katika nchi ambayo watu wake karibu wote ni Waislamu. Tumeona mlango wa injili ukifunguka katika kijiji ambacho asilimia 100 ni Waislamu kwa sababu tu ya huduma hii ya udaktari. Tumeowana vijana wakibadili masisha na kufanyika kuwa wanafunzi wa Yesu- na sasa wanaipelea injili kwa wengi.

Watu wengi ambaao bado wanaishi bila nuru ya injili hawawezi na hawatawakubali wamishenari wanaofanya kazi kiutamaduni, lakini watu hao wanaweza kumkaribisha mtaalamu mwenye taaluma. Wengi wa waliotuletea sisi injili wenye walikuwa ni watu wenye taaluma.

Ujuzi pekee ambaao Mungu hawezi kuutumia ni ule ambao haujatolewa kwake kama kitendo cha ibada. Basi leo nasi tutoe vipawa vyetu na stadi zetu kwa ajili ya umisheni wa kidunia.

Mch. Dk. Joshua Bogunjoko
Mkurugenzi wa Shirika la Umisheni la Kimataifa (SIM International)

UJUZI NA STADI: ZANA MIKONO YA MUNGU

Dk. Bode Olanrewaju ni daktari wa mifugo na mmishenari anayefanya kazi na shirika la CAPRO. Anatumia taaluma yake kuwafikia wale walio katika vizuizi wasifikasiwe na injili katika sehemu za kaskazini mwa Nigeria.

Ni heshima kubwa kutumia maarifa ya udaktari wa mifugo kuwahudumia watu masikini amba maisha yao yanategemea mifugo. Hii imeniwezesha kuwa mfano wa upendo wa Kristo na huruma katika namna inayoonekana.

Msaada wangu wa utaalamu wa mifugo kwa kabile la Wafulani ni daraja la kuanzisha mazungumzo, ambapo vizuizi vya kutokuaminiana na mtazamo hasi walionao watu juu ya wakristo vinavunjwa. Kila mmoja anaweza kutukaribisha kwa upendo kama tu tunaweza kugusa miyo yao. Miyo ya Wafulani inaguswa pale tunapojali makundi yao ya mifugo.

Kila familia kijijini ina kuku. Kiukweli kuku ni kama 'ATM' (mashine ya kutolea pesa benki) ya maskini. Lakini magonjwa huangamiza makundi ya kuku na ng'ombe.

Kwa hiyo, tunawafunza wenyeji na warmishenari kuwa sisi tu watoa kinga au chanjo kwa jamii. Hii imetupa upeno mpana kwenye kaya na imekuza sana kuaminiana. Baadhi ya watu wanadiriki hata kutushirikisha habari za ndani za maisha yao kwa kadiri wanavyoona upendo wa Kristo katika maisha yetu.

Shuhuda kama vile, 'nilipata ada ya shule ya watoto wangu kwa kuuza kuku wa kienyeji', zipo nydingi mionganini mwa wale wanaonufaika na mpango wa mfuko wa shirika la Tearfund kutoka Uingereza, ambalo ni mshirika wetu wa muda mrefu. Uboreshaji wa uzalishaji wa kuku wa kienyeji umekuwa na matokeo mazuri katika kuboresha maisha ya watu.

Muislamu ambaye alikuwa amekataa hata kumsalimia mmishenari mzalendo alibadilisha mtazamo wake pale alipoona kuku wake wamechanjwa na mmishenari na hawakuweza kufa pale magonjwa ya mlipuko yalipotokea. Alikuja na katuomba tukachanje makundi ya mifugo yake!

Leo madaktari wa mifugo, madaktari wa binadamu, wataalamu wa mifumo ya kompyuta na wengineo wanahitajika sana kutumia stadi zao kusaidia wapanda makanisa na kutoa nafuu za maisha kwa jamii zilizopigwa na umaskini. Hata kujihusisha na kazi za umisheni kwa muda mfupi kunaweza kuleta tofauti kubwa.



Jane Banda, Kocha wa mchezo wa pete, hufanya kazi na Sports Friends (Marafiki wa Michezo), ni huduma chini ya SIM inayotumia michezo kama zana kwa ajili ya kubadilisha maisha kupitia injili. Jane anatoka Malawi, ambapo Wakristo wengi hawakuwa na ndoto ya kutumia michezo kama zana ya huduma ya kupeleka injili.

Siku moja Marafiki wa Michezo waliooko Malawi walitambulishwa kwenye kanisa la Jane. Alikuwa ameacha kucheza mpira wa pete kwasababu ya kutoelewana na wazazi wake. Wazazi waliamini kuwa kumruhusu msichana kushiriki katika michezo ni kumpoteza na kuijingiza katika ukahaba.

Marafiki wa Michezo wa Malawi waliwapa wazazi wake habari mpya, na ndipo wazazi wa Jane walipoamua kumwacha Jane ashiriki katika michezo. Sasa Jane ni mmoja wa walimu wa kutumainiwa wa mpira wa pete na anaongoza timu ya mpira ya kanisa lake.

Watoto wengi wanampenda Jane na huduma yake ya michezo. Baadhi ya watoto anaowafundisha wamemwamini Yesu na sasa ni sehemu ya kanisa. Wazazi wake Jane wanafurahi kwa sababu Jane anaendelea kuifikia jamii kwa ajili ya Kristo.

Hadithi ya Jane inamkumbusha andiko lisemalo: 'Jiwe lililokataliwa na mjenzi siku moja likuwa jiwe kuu la pembedi'. Michezo ambayo ilidhaniwa kuwa ni kitu kibaya na kingeleta tabia mbaya, bali sasa ni zana kubwa ya kubadilisha maisha! Ni kweli Jane anajishughulisha na kazi za kanisa na kuigusa familia yake. Pia ana furaha ya kuwaona wanajamii wakimwamini Kristo.



Mch. Edwin Fussi ni mmishenari mwenye historia ya kuwa mfanyakibashara; alimiliki duka dogo kabla ya kusoma shule ya umishenari na kuanza kazi ya umisheni katika makundi ambayo bado hayajafikiwa na injili nchini Tanzania.

“Familia yangu ilipofika katika jamii ambayo tunatumika sasa, asilimia 99.9 walikuwa ni Waislamu. Kulikuwa na vikwazo vingi dhidi ya injili. Tulikataliwa, tulitukanwa na kudhihakiwa. Nilitambulishwa kwa wanakijiji kama mchungaji, mwalimu na kiongozi wa dini ya kikristo. Mkakati wetu ulikuwa wa uinjilisti wa nyumba kwa nyumba, lakini jamii ilitukataa.

Vijana walitukimbia walipotuona wakidhani sisi ni wapelelezi wa serikali. Viongozi wa misikiti waliwazuia watu wasichangamane na sisi ili wasiwe Wakristo. Baadhi ya watu walituambia kuwa ‘sisi tuna dini yetu na wao wana dini yao.’ Tulimwomba na kumsubiri Bwana. Kulikuwa na changamoto ya makanisa yalijotutuma kupunguza msaada wa kipesa baada ya kuona hakuna matokeo na watu kujiondoa kwenye kikundi cha waombaji. Nilanza kufikiri kuwa ingekuwa vema kama ningeiacha kazi hii—maana ningerudi nyumbani na kuendelea kuhubiri injili na huku nikiendelea na biashara zangu.

Lakini siku moja nilipokuwa nasoma Biblia, Mungu alinionyesha jinsi Mtume Paulo alivyoweza kutumia ujuzi wake katika huduma. Bwana aliniambia, “unaweza kuendelea kunitumikia katika kijiji hiki na kushinda changamoto kama tu utatii na kutumia ujuzi niliookupa.” Nilisema, “asante Bwana. Najua jinsi ya kuendesha biashara. Je, inawezekana kuanza biashara hapa na huku nikiendelea na malengo ya kuwafikia watu kwa injili?”

Kwa mtaji mdogo, nilanzisha duka dogo la kuuza vifaa vya umeme wa jua na vinywaji. Nilikuwa nachaji simu za mkononi na betri pamoja na biashara ya kunyoa nywele. Baada ya miezi michache niliweza kutengeneza marafiki wengi. Wanakijiji walilacha kutufikiria sisi kama maadui. Hapakuwa na umeme katika kijiji chetu kwa wakati huo, lakini waliweza kuchaji simu zao na kununua vifaa vya umeme wa jua na kunitaka mimi niwakeeke mfumo wa umeme. Niliweka mistari ya Maandiko katika taa zote nilizowafungia. Uendeshaji wa biashara uliondoa vikwazo vingi vilivyokuwepo, na ilitusaidia kujenga daraja imara la kuyafikia makabila katika eneo hilo.

Msanifu wa Majengo, Tito Oludotun Kumapayi ni mkurugenzi wa shirika la Umisheni na Uinjilisti kwa makanisa ya Nigeria, Usharika wa Kianglikana. Ana ofisi ya usanifu majengo katika mji wa Ibadani, mahali ambapo anaishi na mke wake, Margaret.


Mwaka 1991, nikiwa katika chuo cha Hagai huko Singapore, nilishawishika kuwa nisiwekwe wakfu kuwa mchungaji bali niendelee na kazi yangu ya Usanifu Majengo na niitumie kwa ajili ya uinjilisti, kuleta roho kwa Kristo na kuwafanya watu kuwa wanafunzi wa Yesu.

Kwa hiyo, katika ofisi yangu, kila siku nilianza na maombi na kusoma Biblia kwa muda wa dakika kama 30 hivi. Kwa kadiri ushirika huo ulivyoendelea kukua, baadhi ya wafanyakazi walikuja kwangu na kutafuta ushauri kuhusu masuala ya kazi na ndoa. Baada ya muda mfupi ushirika wetu ulianza kusafisha wafanyakazi wetu kwa maana ya kujitoa zaidi kufanya kazi na kusimamia miradi. Ofisi yetu ilianza kuvutia wakristo waliotaka miradi yao ifanywe vizuri.

Wakati mmoja tulipokuwa tunasimamia mradi wa serikali, mmoja wa wajenzi wetu ambaye ni muislamu mmoja alikuja na kusifia kazi na jinsi kazi yetu ilivyokuwa inakwenda vizuri. Baadaye alikuja kwangu na kuamua kutoa maisha yake kwa Kristo. Muislamu huyu aliyebadilika na sasa anatumika kama Shemasi katika kanisa la mtaani kwao.

Kama ambavyo madhabahu ni kwa mtumishi aliywewkwa wakfu, ndivyo ilivyo mahali pa kazi kwa mkristo mwenye taaluma. Mtu mwenye taaluma anaweza kupakwa mafuta kuhudumu katika mazingira yake kwa ajili ya ukuaji wa ufalme wa Yesu Kristo. Mara kadhaa nawaambia watu kwamba kazi halisi ni kuleta roho kwa Kristo na kuwafanya watu kuwa wanafunzi wa Yesu, ilahli kazi ya usanifu majengo ni ya muda tu.





KUMTUMIKIA MUNGU KUPITIA TAALUMA YAKO ITAKUWAJE MUNGU AKIUITA KUWA MSANIFU MAJENGO? FEMI B. ADELEYE

Kwa sababu mahali pa kazi ndipo tunapotumia muda wetu mwingu katika juma, ni fursa nzuri kwa kufanya huduma.

Katika miaka yangu ya kufanya kazi pamoja na wanafunzi, baadhi yao hutaka ushauri wangu wanapokuwa wanaomba na kufunga ili kuanzisha kanisa au kuijunga na shirika la umisheni. Na wakati mwagine huwa nawauliza "Je, vipi kama Mungu anakuita uwe msanifu majengo au mhandisi? Jibu lao hao, 'lakini hiyo ni kazi tu. Wangependa kunikumbusha juu ya Waefeso 4: 11, maneno yanayotumika kusisitiza kuwa huduma halisi ni ile ambayo hufanywa na mitume, manabii, wainjiliisti, wachungaji na walimu.

Hapo mimi hupenda kueleza kuwa kusudi la karama za huduma ni kutuandaa kwa ajili ya utumishi. Wakati wengine wataitwa kuwa wachungaji, wainjiliisti na wamishenari, wengi wetu wataitwa kuwa walimu, wafanyabiashara, mafundi, na wasimamizi wa kazi, na wengineo wengi.

Watu wengi hufikiri kumtumikia Mungu ni kufanya kazi za kanisani au umisheni tu. Lakini karama zilizoorodheshwa katika Waefeso 4:11 siyo njia pekee za kumtumikia Mungu. Zipo njia nyingine kama vile kutiana moyo, ukarimu, matendo ya huruma (Warumi 12:8) au kuwasaidia watu (1 Wakorintho 12: 8) zote zina umuhimu sawa.

Tofauti mbili zisizotusaidia

Maana tu kazi ya Mungu, tumeumbwa katika Kristo Yesu ili tutende matendo mema, ambayo tokea awali alituandaa ili tuyatende' (Waefeso 2:10). Kwa hiyo, miito yetu ya kitaaluma imewekwa wakfu kabla ili iweze kumtumikia Mungu. Kama hatuwezi kushukuru kwa hili, basi

tutakuwa tumeshawishiwa na upande mmoja kati ya pande zisizo na afya.

Kwa hiyo taaluma zetu ziandaliwe kuwa eneo la kuendeleza utumishi kwa Mungu. Kama hatuwezi kuikubali hii, itakuwa ni kwa sababu tumeshawishiwa na mojawapo ya tofauti au zote mbili.

Baadhi ya watu hufikiri kuwa utumishi wa kikristo hufanyika kwa msingi wa mikutano ya kikristo, na siyo katika uwanja wa hadhara.

Maisha yote ni Matakatifu

Matokeo yake ni kwamba, baadhi wanaamini kuwa tunawajibika katika eneo la kiroho tu. Lakini kile ambacho tunafikiri kuwa ni cha kidunia huwa na matokeo muhimu kwa umisheni na mabadiliko kwa ujumla. Kwa mfano siasa siyo tu ni siasa za kidunia pale serikali isiyojali haki inapozua haki kwa maskini au kuzuia uhuru wa kuhubiri injili.

Tunahitaji kuwa na mtazamo wa Kiebrania wa kuona kuwa maisha yote ni kitu kitakatifu. Katika Agano la Kale Mungu anaonyesha haja yake ni kwa namna gani utawala, kilimo, usanifu majengo na viwanda na masoko vinavyopaswa kufanyika. Kuna miongozo mitakatifu ya mahusiano ya kimataifa, ya kijamii na masuala yote ya maisha ambayo tunaweza kuyaweka katika kundi la mambo ya kidunia leo.

Napendekeza sababu tatu, mionganoni mwa nyingi, kwa nini ni muhimu kumtumikia Mungu kupidia taaluma zetu. Kwanza, huu ulimwengu ni mali ya Mungu na ye ye anahusika na jinsi tunavyoutawala. Kama vile alivyompa Adamu na Hawa wajibu wa kuitunza Bustani ya Edeni, ndivyo anavyotuita sisi kuwa mawakili wa uumbaji kupidia taaluma zetu.

Pili, mahali pa kazi zetu za kitaaluma ni mahali pa kuwashuhudia wengine habari za Yesu. Hatuwezi kufanya haya kwa kugawa karatasi zenyenje ujumbe wa Mungu, bali pia kwa kupidia kujitoa kwetu na kwa juhudhi yetu, kufanya kazi kwa bidii na kwa ufanisi. Tufanye kazi zetu za kitaaluma kama vile tunafanya kwa Mungu. Kama tusomavyo maandiko, Yusufu alitumikia makusudi ya Mungu kama msimamizi wa masuala ya uchumi wa Misri; Daudi kama mchungaji na mfalme katika Israeli, Nehemia kama mnyweshaji wa mfalme; na Lidia kama mushona nguo za zambarau.

Tatu, matatizo mahali pa kazi husababishwa na uzembe, kuto kujali, tamaa, au ujisadi. Hali hii ni sababu ya kuhitaji wakristo wenye wito katika kusudi la Mungu kwa moyo wa shukrani sana kupidia taaluma na maarifa waliyonayo. Hasara ya maisha ambayo husababishwa na wahandisi wana opitisha majengo ambayo yana kasoro au wafamasia wanaouza dawa zilizopitwa na muda wa matumizi ni kiashirio tosha cha hitaji kwa wakristo wanataluma.

Wakristo waaminifu wanapomtumikia Mungu kupidia taaluma zao, ukuu wa Kristo huonekana katika nyanja zote za maisha.

Femi B. Adeleyeni mkurugenzi mtendaji wa taasisi ya Mguso wa kikristo (Institute for Christian Impact) huko Ghana na ni Mkurugenzi mshiriki wa Afrika wa Langham Preaching. Kabla ya hapo alifanya kazi na shirika la World vision na kabla ya kuijunga na world vision alifanya kazi kwa miaka 23 na International Fellowship of Evangelical Students (Ushirika wa kimataifa wa wanafunzi wa kiinjili). Mke wake anaitwa Affy na wana watoto wanne.

NENDA!

HABARI ZA KANISA LA AFRIKA LINALOHAMASISHA

BASI NA TUSIKIE KUTOKA KWAKO

Je, una maswali kuhusu somo hili au mada zingine kuhusu umisheni? Ni masuala gani ungependa AfriTwende ikuletee?



Tunakaribisha mawazo yako, ili tuweze kuboresha jarida letu liweze kutimiza lengo lake kwa ukamilifu iwezekanavyo. Tafadhalii tuma baruaapepe kwa: afritwende@afriko.org

Pia tunachapisha habari na taarifa za wamishenari sambamba na nukuu za kusisimua katika kurasa zetu mpya za mitando ya kijamii. Tutembelee kwenye Facebook kwa www.facebook.com/afritwende na Instagram kwa www.instagram.com/afritwende. Pia unaweza kujipakulia taarifa zetu zote kwa tovuti ya www.afriko.org/afri-twende.

MAFUNZO YA UMISHENI

East Africa School of Mission (EASM) ni chuo kilicho chini ya bodi ya wachungaji ya mafunzo ya utume. Inayotoa mafunzo ya umisheni kuanzia ngazi ya cheti, diploma na shahada. Chuo hiki kilianza 2015 kama shule ya utume ya kwanza nchini Tanzania, mkoa wa Dar es salaam. Lengo la kutoa mafunzo ya umisheni yaani utume wa kuwafikia wasiofikiwa.

Chuo kilianza kutoa wahitimu wa umisheni wa kuwafikia wasiofikiwa. Wachungaji, Wainilistini na Maaskofu waliojiunga kwa mwaka 2015 kwa ngazi zote zilizotajwa hapo juu ambao walipata umaarufu mkubwa kama

MAPITIO YA KITABU CHA UMISHENI

Umisheni wa kuwafikia wale ambao hawajafikiwa

Kwa hakika hiki ni kitabu kizuri sana cha Umisheni, kinachopatikana katika lugha ya Kiswahili.

Kitabu hiki ni ufupisho wa masomo yanayofundishwa katika semina hizo za uhamasishaji na katika masomo ya utangulizi wa umisheni chuoni. Kinajumuisha mada za; Umisheni wa Kibiblia, Historia ya Umisheni, Jinsi ya kutumika katikati ya watu wa utamaduni tofauti na wa kwako, Mbinu na mikakati ya kuwafikia wale ambao hawajafikiwa.

Hiki ni kitabu kizuri mno kwa kufundishia katika lugha ya Kiswahili. Unaweza kukinunua sasa kwa kuwasiliana na Mkuu wa Chuo cha Umisheni cha Afrika ya Mashariki.

Kitabu kinauzwa kwa sh. 3000/, kinafaa sana kwa matumizi ya kufundishia waumini, watumishi, wanafunzi wa vyuo vya umisheni, vyuo vya Biblia n.k.

Kwa mawasiliano +255754615853 <kengelasam@gmail.com> Karibuni sana na Mungu wa Mbinguni awabariki sana.



wachungaji wenye elimu na uwezo mkubwa katika ufahamu wa utume wa kuwafikia wasiofikiwa kwa Afrika.

Mwaka 2016, chuo kilihamia katika majengo ya chuo cha kanisa la Kibatisti kinondoni B. Hii ilisababishwa na umbali uliokuwepo kwa wanafunzi wa kutwa kufika vikindu na kurudi mjini, na miundo mbinu kutokuwa rafiki sana kwa wakati huo. Mwaka 2017, chuo kilihamia Pugu Kajiungeni katika majengo ya kanisa la Shinglight Church, ambapo ndio kipo mapaka sasa. Hii ni kutohana na wanafunzi kuongezeka. Masomo ya vitendo ya

ujasilia mali yalaianzishwa (kushona mahema) mafunzo haya hutolewa kwa mwaka mmoja kwa ngazi zote.

Chuo kimeendelea kuka na kutanuka na kupata umaarufu mkubwa ndani na nje ya ya mipaka ya Tanzania. Chuo kiliendelea kutoa mafunzo bora sana kwa wamishenari, wainjilisti na wachungaji, yanayohusu utume/umisheni wa kuwafikia wasiofikiwa. Chuo kimekuwa na wanafunzi kutoka Tanzania, Burundi, Congo ya DRC, Sudan kusini n.k. Chuo kina mabweni na madarasa pamoa na walimu wa uhakika kutoka ndani na nje ya Tanzania na Afrika.

Karibu ujiunge nasi, mawasiliano yetu ni;

- Bishop Eliasaph Mattayo: +255655501202 eliasaph.mattayo@gmail.com (Mwnyekiti)
- Mch. Samwel Kengela: +255754 615853 kengelasaam@gmail.com (Mkuu wa chuo)

MAKUNDI YA WATU WATOPOSA

Watoposa ni jamii ya wakulima na wafugaji wanaoishi Sudani ya Kusini, wanaokadirwa kufikia idadi ya watu 500,000. Watu hawa wanategemea ng'ombe, kondoo, na mbuzi. Wavulana huchunga mbuzi na kondoo na huacha kuchunga ng'ombe wakifikia umri wa mkubwa. Wakati wa masika wanyama wanachunga karibu na vijiji. Mvua zinapokoma, wanaume hupeleka makundi ya mifugo kwenye maeneo malisho wakati wa kiangazi na huwarudisha mvua zinapoanza. Watoposa pia wanafanya shughuli ya kuchenjua dhahabu na madini mengine.

Kila tukio kubwa la kijamii huhusisha kutolewa kwa ng'ombe kama malipo au ahadi. Hali hii huweza kusababisha msuguano kati ya majirani pale ambapo hakuna ng'ombe wa kutosha kwa ajili ya mahari ya mke wa kwanza. Wanasiifika kama watu wenye tamaa kubwa ya umiliki wa ng'ombe kuliko makabila jirani. Mtu ambaye anaweza kutoa ng'ombe wengi hasa kwenye kipindi cha vita, hupewa heshima ya juu.

Utarwala wa kisiasa ndani ya watoposa hauko wazi, ingawa wazee, machifu na watu wenye busara hupewa heshima. Maamuzi katika ngazi ya ukoo au jamii hufanywa kwenye

mikutano ambayo huwa inahudhuriwa na wanaume pekee. Wanawake hubakia nyumbani kulima, kupika na kulea watoto.

Utamaduni wa Watoposa huendelezwa kwa njia ya mdomo kama nyimbo, ngoma, muziki, mashairi, na hadithi. Watoto wengi wa jamii ya watoposa sasa wanakwenda shule, lakini kiwango cha kujua kusoma na kuandika kiko chini.

Wanaweza kufikiwaje na injili?

Watu hawa wanaamini katika miungu na viumbe fulani kuwa vina uwezo kama vile roho za mababu zinasaidia matatizo yao ukame na milipuko ya magonjwa ya mifugo. Imani hizi zinaunganishwa pamoja na katisimu ya wakatoliki, pamoja na hirizi na imani juu ya dini zinazoamini kuwa watu wanakuwa kama walivyojaliwa na hawawezi kubadilika.

Idadi ya Wakristo Watoposa ni chini ya asilimia moja. Wamissionari wametumia mafunzo ya ufuasi na masimulizi ya Biblia ambayo yamekuwa yanatolewa na viongozi waliofundishwa. Watu wenye moyo wa utumishi pamoja na taaluma katika maeneo kama udaktari, mifugo, kilimo na maji wanatakiwa ili kuwafikia watoposa na injili. Wamishenari wachache kutoka Kenya wamekuwa wakifanya kazi huko.

MWOMBE MUNGU ILI:

- Atume wamissionari wenye ujuzi wa kilimo, udaktari na udaktari wa mifugo kuwapelekea watoposa injili.
- Wawepo watafasiri ili watu wapate Biblia katika lugha zao za kwanza.

- Atoe watendakazi wa injili ambao wana ujuzi katika kufundisha maandiko kwa njia ya mazungumzo.
- Awasaidie Watoposa kuendeleza mahusiano mazuri miongoni mwao na majirani.



AFRITWENDE: afritwende@afrigo.org **AFRIGO:** info@afrigo.org **ALLONS-Y !** : info@afrigo.org **AFRÍDE :** afride@afrigo.org

SIM East Africa
Tel: +251 911 206 530
east-africa.office@sim.org

SIM West Africa
Tel: +233 30 222 5225
wamo.personnel@sim.org

SIM Southern Africa
Tel: +27 21 7153200
za.enquiries@sim.org

AIM International
amc.io@aimint.org
aimint.org/africanmobilization/